GCCTC

**GENDER AND CLIMATE CHANGE TANZANIA COALITION (GCCTC)**

# KUJUMUISHA MASUALA YA KIJINSIA KATIKA SERA, MIKAKATI, NA MIPANGO YA MABADILIKO YA TABIA NCHINI TANZANIA: UCHAMBULIAJI WA HARAKA

## UTANGULIZI

Ndugu wadau.

Ninayo furaha kubwa na shukrani za kipekee kuwaletea muongozo Muhimu wa Jinsia na Mabadiliko ya Tabianchi unaozingatia Usawa wa Kijinsia katika Sera, Mipango, na Mikakati ya Tanzania.

Kama Mratibu wa Taifa wa GCCTC, ninafurahi kushiriki katika kuuandaa muungozo huu muhimu, ambao umeandaliwa kwa ustadi na mshauri elekezi aliyejitolea.

Napenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa Shirika la Gender Response Resilience and Intersectionality in Policy and Practice (GRRIPP- Afrika), chini ya uongozi wa Profesa Cheryl Potgieter (GRRIPP Afrika) na Profesa Maureen Fordham (GRRIPP UCL, London) kwa uongozi wao na uungaji mkono usio na shaka.

Kujitolea kwao kumekuwa chachu katika kutuwezesha sisi kusukuma hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi zinazozingatia usawa wa kijinsia nchini Tanzania, sambamba na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), na kuendeleza malengo yaliyoainishwa katika mpango mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Muongozo huu una mambo muhimu yanayotumika kama mwongozo kamili, ukifungua macho utaona mwingiliano usiopingika kati ya jinsia na mabadiliko ya tabianchi katika muktadha wa Tanzania.

Tunaamini kwamba ufahamu unaoelezwa hapa sio tu utaongeza uelewa bali pia utachochea hatua za maana kuelekea mustakabali wenye usawa na endelevu zaidi.

Asante kwa ushirikiano wenu wa kudumu na kujitolea kwenu katika kuendeleza usawa wa kijinsia na uthabiti wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Salamu za dhati,

Maria

Maria Matui
Mratibu wa Taifa,
Muungano wa Tanzania wa Jinsia na Mabadiliko ya Tabianchi (GCCTC)

## 1. USULI

Mabadiliko ya tabia nchi ni moja ya changamoto kubwa zaidi katika karne ya 21, zenye athari kubwa kwa jamii za binadamu na mifumoikolojia duniani kote. Athari za mabadiliko ya tabianchi zinaonekana kimataifa, zikivuka mipaka ya kijiografia na kuzigusa jamii mbalimbali. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kuwa athari za mabadiliko ya tabia nchi si sawa kwa jinsia zote; wanawake na wanaume mara nyingi huathirika kwa njia tofauti.

Sehemu mbalimbali duniani, ikiwa ni pamoja na Tanzania, wanawake wanalo jukumu muhimu sana katika usimamizi wa rasilimali asilia, kufanya shughuli za kilimo, na kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula. Jukumu hili linalowafanya kuwa tegemezi kwa sehemu kubwa kwenye sekta zinazoathiriwa na hali ya hewa (Massoi. L.W, 2019). Licha ya hili, wanawake mara nyingi wanakabiliwa na vikwazo vya kijamii, kiuchumi, na kitamaduni vinavyopunguza uwezo wao wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa ufanisi. Tofauti za kijinsia, upatikanaji wa rasilimali usio sawia, na ushiriki mdogo katika mchakato wa kufanya maamuzi vinaongeza hatari ya wanawake kuathiriwa zaidi na mabadiliko ya tabianchi.

Tanzania, iliyoko Afrika Mashariki, ni nchi yenye mifumoikolojia mtambuka na urithi wa kitamaduni wenye utajiri wa kipekee. Ni nchi yenye jamii mbalimbali ambazo maisha yao yanahusiana sana na mazingira na rasilimali asilia. Kwa kutambua athari za kijinsia za mabadiliko ya tabianchi, serikali ya Tanzania imejitahidi kujumuisha mtazamo wa kijinsia katika Sera, Mikakati, na Mipango yake inayohusu mabadiliko ya tabianchi. Hatua hizi zinalenga kukuza usawa wa kijinsia, kuwezesha wanawake, na kuimarisha uhimili wa mabadiliko ya tabianchi miongoni mwa jamii zinazoathirika zaidi.

## 2. UTANGULIZI

Kujumuisha masuala ya jinsia katika sera, mikakati, na mipango ya mabadiliko ya tabianchi ni hatua muhimu kuelekea kutoa majawabu yenye ufanisi, usawa, na endelevu katika kutatua changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Kwa kutambua tofauti iliyopo kimajukumu, kimahitaji, na kiuzoefu kati ya wanawake na wanaume, watunga sera wanaweza kubuni afua zenye shabaha ya kushughulikia hatari mahususi au kutumia fursa mahususi zinazohusiana na jinsia tofauti katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Ripoti hii fupi inaiangazia Tanzania ili kuonyesha ni kwa kiasi gani masuala ya kijinsia yamejumuishwa katika sera kuu za mabadiliko ya tabia nchi, mikakati, na mipango ya kitaifa. Lengo ni kutathmini maendeleo nah atua iliyofikiwa katika kukuza usawa wa kijinsia na kuwezesha wanawake katika muktadha wa mabadiliko ya tabia nchi, pamoja na kutambua mapengo na changamoto katika utekelezaji.

Ripoti itachambua sera na mikakati muhimu ya mabadiliko ya tabia nchi nchini Tanzania, ikionyesha hatua na mikakati maalum inayojumuisha masuala ya jinsia katika sera husika. Pia, itachunguza mgawanyo wa rasilimali za bajeti kwa miradi inayohusiana na

jinsia ndani ya sera hizi, kujaribu kuelewa kiwango cha dhamira ya kufadhili mikakati hiyo kuelekea kuleta usawa wa kijinsia katika juhudi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Zaidi ya hayo, ripoti itazingatia matokeo na athari za sera za mabadiliko ya tabianchi zinazojumuisha masuala ya jinsia, ikichunguza ufanisi wake katika kusaidia ushiriki wa wanawake, kuongeza upatikanaji wa rasilimali, na kujenga uhimilivu wa tabianchi kwenye ngazi ya jamii.

Kwa kuangazia mafanikio na changamoto vya ujumuishaji wa jinsia katika jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi nchini Tanzania, ripoti hii inalenga kutoa elimu kwa watunga sera, wataalam, na wadau mbalimbali wanaochangia jitihada za kujenga uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi na usawa wa kijinsia katika ukanda wa Afrika Mashariki na kwingineko.

## 3. UCHAMBUZI JUU YA KUJUMUISHA JINSIA KATIKA SERA, MIKAKATI, NA MIPANGO YA MABADILIKO YA TABIA NCHI NCHINI TANZANIA

Tanzania inatambua kuwa athari za mabadiliko ya tabianchi hazina usawa wa kijinsia na zinaweza kuwagusa wanawake na wanaume kwa namna tofauti. Kutambua hili, serikali ya Tanzania imechukua hatua kadhaa kujumuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika sera zake, mipango na mikakati ili kuhakikisha upo mfumo jumuishi na sawia katika kushughulikia mabadiliko ya tabianchi. Ufuatao ni muhtasari kuhusu ujumuishajiw amasuala ya kijinsia katika maandiko ya sera muhimu za mabadiliko ya tabianchi nchini Tanzania.

**Muhtasari wa Mambo ya Kijinsia katika Sera, Mikakati, na Mipango ya Mabadiliko ya Tabiachi nchini Tanzania**

| Na | Sera/Mikakati/Mipango | Mambo ya Kijinsia yalivyojumuishwa | Bajeti | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Programu ya Kitaifa ya Kuboresha Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (National Adaptation Programme of Action -NAPA, 2007) | Haisemi kitu chochote kuhusu jinsia na mabadiliko ya tabianchi | Hakuna bajeti iliyotajwa kwa sababu hakuna masuala ya kijinsia yaliyotajwa | Sekta zinazotambulika kwamba zinaathirika zaidi na mabadiliko ya tabianchi |
| 2. | Mkakati wa Kitaifa wa MKUHUMI (The National REDD+ Strategy -2012) | a) Inatambua umuhimu wa usawa wa kijinsia katika uhifadhi wa misitu.<br>b) Inalenga kushughulikia tofauti zinazotokana na jinsia katika kupata rasilimali za | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | misitu na kufanya maamuzi yanayohusiana na usimamizi wa misitu.<br>c) Inaendeleza ushiriki wa wanawake katika juhudi za MKUHUMI na inatambua jukumu kubwa wanalolibeba kama walinzi wa misitu.<br>d) Inapendekeza maendeleo ya mwongozo wazi unaojumuisha masuala ya jinsia kuhusu umiliki wa ardhi. | | |
| 3. | Mwongozo wa Kitaifa wa Kuimarisha Usawa wa Jinsia katika Mabadiliko ya Tabianchi (National Guidelines for Mainstreaming Gender into Climate Change - 2014) | Mwongozo unapendekeza yafuatayo:<br>a) Kuongeza uwezo wa wanawake katika usimamizi wa mazingira;<br>b) Kuchochea usawa wa jinsia katika usimamizi wa mazingira na mgawo wa faida zitokanazo na huduma za mazingira;<br>c) Kuhakikisha, haki za wanawake zinaheshimiwa na kuna mgawanyo sawia wa gharama na faida zitokanazo na usimamizi wa mazingira;<br>d) Kutumia fursa za masuala ya jinsia katika sheria na sera za kimataifa na za kitaifa;<br>e) Kuhamasisha mazoea bora ya kuimarisha usawa wa jinsia katika usimamizi wa mazingira. | 0 | Unapendekeza kwamba vipengele vya kijinsia vingeingizwa katika mipango na bajeti zilizopo kadri inavyowezekana ili kuongeza ufanisi |
| 4. | Sera ya Nishati ya Kitaifa (The National Energy Policy -2015) | a) Inaelekeza kuwepo na uswa katika upatikanaji wa vyanzo vya nishati safi na nafuu kwa wanaume na wanawake.<br>b) Inalenga kupunguza mzigo wa majukumu yanayohusiana na nishati kwa wanawake kwa kukuza matumizi ya teknolojia za nishati safi na za kisasa na kuboresha mazoea ya jadi.<br>c) Inaelekeza uwepo ushiriki wenye tija wa wanawake na | 0 | Hakuna maoteo ya bajeti katika ngazi ya Sera |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | wanaume katika mchakato wa kufanya maamuzi. | | |
| 5. | Sera ya Mazingira ya Kitaifa (National Environmental Policy -2021) | a) Inatambua kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia katika upatikanaji na udhibiti wa rasilimali asilia. b) Inatambua kwamba kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia kunadhoofisha mafanikio ya mikakati na programu za kitaifa za uhifadhi wa mazingira. c) Inatambua umuhimu wa usawa wa kijinsia kama sehemu muhimu katika usimamizi wa mazingira na maendeleo endelevu. d) Inahimiza kuunganisha vipengele vya kijinsia katika usimamizi wa mazingira. e) Inaita kwa kuhamasisha uelewa wa umma juu ya jukumu la kijinsia katika uhifadhi wa mazingira. | | Hakuna maoteo ya bajeti katika ngazi ya Sera |
| 6 | Mkakati wa Kitaifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (National Climate Change Response Strategy - NCCRS, 2021-2026) | a) Unatambua kwamba mabadiliko ya tabianchi yanawaathiri wanawake na wanaume na namna tofauti.<br>b) Unalenga kukuza hatua za kupunguza na kuhimili mabadiliko ya tabianchi zinazozingatia masuala ya kijinsia.<br>c) Unalenga kuwawezesha wanawake kwa kuwajumuisha katika mchakato wa kufanya maamuzi, kuboresha upatikanaji wao wa rasilimali, na kutambua jukumu lao katika kuhimili mabadiliko ya tabianchi. | Tsh. Bilioni 5 kufikia 2026 | Wizara inayoshughulikia masuala yay a jinsia, elimu, mazingira, ardhi, Serikali za Mtaa, Mifugo, Kilimo, Uchukuzi, Uvuvi, Maji, Nishati, Madini, Maliasili; NEMC; TMA, Taasisi za Tafiti na Elimu;<br>Taasisi za kijamii na Sekta binafsi |
| 7 | Mchango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (Nationally Determined Contributions - 2021-2030) | a) Unakuza na kuimarisha usawa wa kijinsia katika hatua za kukabiliana na kwa mabadiliko ya tabianchi. | Dola za Marekani 8,000,000 kwa sekta zote | Wizara inayoshughulikia masuala yay a jinsia, elimu, |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | b) Unakuza hatua za kushughulikia athari hasi za mabadiliko ya tabianchi kwa vijana, wanawake, wazee, na makundi mengine yaliyotengwa, ikiwa ni pamoja na watu wenye ulemavu. | (6,500 Bara na 1,500 Zanzibar) | mazingira, ardhi, Serikali za Mtaa, Mifugo, Kilimo, Uchukuzi, Uvuvi, Maji, Nishati, Madini, Maliasili; NEMC; TMA, Taasisi za Tafiti na Elimu; Taasisi za kijamii na Sekta binafsi |
| 8 | Mpango wa kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Sekta ya Kilimo Tanzania (Tanzania Agriculture Climate Resilience Plan, 2014–2019) | Chini ya mpango huu, kuna Mpango wa kufanya tathmini kamili kuhusu masuala ya jinsia na mabadiliko ya tabianchi katika sekta ya kilimo, ikiwa ni pamoja na:<br><br>a) Athari za mabadiliko ya tabianchi kwa wanawake na wasichana<br>b) Kuandaa mapendekezo na mwongozo wa kuingiza vipengele vya kijinsia katika Sera, Mikakati, Programu, na bajeti zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi katika maeneo husika ya mamlaka<br><br>c) Kutambua mazoea bora nchini Tanzania na nchi nyingine,<br><br>d) Kutambua teknolojia zinazofaa kwa shughuli zinazohusiana na usimamizi wa maji, kilimo kinachozingatia mabadiliko ya tabianchi, na usindikaji na kuongeza thamani baada ya mavuno,<br><br>e) Kuimarisha uwezo na kuongeza uelewa kuhusu mabadiliko ya tabianchi kwa wanawake wakulima, | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | f) Mapendekezo ya kuongeza upatikanaji wa rasilimali za kifedha na uzalishaji kwa wanawake. | | |
| 9. | Mpango Kabambe wa Mazingira wa Taifa wa kufanya Afua za Kimkakati (National Environmental Masterplan for Strategic Interventions 2022-2032) | a) Unatetea uwezeshaji wa jinsia na ujenzi wa uwezo;<br>b) Unapanga kuendeleza na kutekeleza programu ya uwezeshaji wa jinsia kwa biashara ya kaboni ifikapo mwaka 2025 | Hakuna bajeti | Mpango unapendekeza afua tu. Watekelezaji watapanga bajeti kulingana na aina na ukubwa wa afua walizochagua kutekeleza |

**Hitimisho**

Kutokana na uchambuzi huu, inaonekana wazi kwamba Tanzania imefanya hatua fulani katika kutambua umuhimu wa jinsia katika shughuli zake mbalimbali, ikiwa ni pamoja na hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Taifa limejikita katika kuingiza vipengele hivi katika sera zake kuu za mabadiliko ya tabianchi, mipango, na mikakati mingine ya maendeleo ambayo inaweza kuwa na mchango wa moja kwa moja katika hatua za kitaifa za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Juhudi hizi zinalenga kuimarisha usawa wa kijinsia, kuwawezesha wanawake, na kujenga uhimili wa mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea kujitokeza.

Hata hivyo, bado kuna changamoto. Licha ya mfumo wa kisera, mageuzi ya kisheria, na miundo ya kisheria na kitaasisi iliyoanzishwa kushughulikia pengo la jinsia, kuna haja ya kujua ni kwa kaisi gani hatua hizi zinatekelezeka katika ngazi zote za serikali. Kuna haja ya kuwepo njia ya wazi ya kuonyesha ni jinsi mipango na bajeti zinazingatia masuala ya jinsia, jinsi gani mgawo wa bajeti za programu mbalimbali zinawanufaisha wanawake na wanaume kwa usawa, ikiwa ni pamoja na makundi mengine yanayoathirika zaidi. Utafiti wa kina katika sekta muhimu unahitajika kufanywa ili kutathmini ni kwa kiasi gani mambo ya jinsia yamejumuishwa, ni hatua gani maalum zimepangwa, nini kinachofanyika, na ni matokeo gani yanayopatikana. Ahadi endelevu, uhamasishaji, na ushirikiano kutoka kwa wadau wote utakuwa muhimu kuhakikisha mafanikio ya sera za mabadiliko ya tabianchi zinazojumuisha masuala ya kijinsia nchini Tanzania.

*Hosted by: Gender and Climate Change Tanzania Coalition*
*P.O Box 3710*
*Dar es Salaam, Tanzania*
*Mobile: 0679 933 022*
*Email:gcctctz@gmail.comOR  info@gcctc.or.tz*

GCCTC